بسم الله الرحمن الرحيم

| |
|---|
| Jumaatano 5/Jumaadal Aakhira/1428 H =20/06/2007 AD<br>Pongwe-Tanga,Tanzania.makala namba 15. |

# HII NDIYO DAAWA YETU

# JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

MJUE IMAM MUHADDITH KATIKA NCHI YAYEMEN
KATIKA ZAMA HIZI

MUQ'BIL IBN HAADI IBN MUQ'BIL AL HAMDAANY AL WAADI'I
Allah amrehemu.

| |
|---|
| Amesema al Imamu Shk Muhammad Swaleh Ibn Uthaimin r.a;<br>قولوا له: أنا أعتبره مجدداً<br>Mwambieni (Muq'bil) mimi nina mzingatia yeye kuwa ni Mujaddidi (wa Yemen)<br>Tazama Nubdhatun Mukh'taswara min Naswaih.. uk 46. |

MUANDISHI;

AL AKH ABUL FADH'LI QASSIM MAFUTA QASSIM.

بسم الله الرحمن الرحيم

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote,na shukrani zote.
Ni zako wewe sifa njema vile zinavyolingana na utukufu wako,na ukubwa wako,ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike,na pale unaporidhika, na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake,na maswahaba zake wote,na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Ama baada ya utangulizi huu wa kheri,ndugu msomaji huu ni mfululizo wa makala zetu ambazo miongoni mwa malengo yake ni kuwaelimisha watu thamani na nafasi ya maulamaa wa Ahli Sunna wal Jamaa na kuwatetea pale wanapo dhulumiwa kwa kusingiziwa au kutuhumiwa kwa mambo wasiyokuwa nayo.

Limekuwa ni jambo la kawaida sasa kwa Mudir wa Ansaar Muslim Youth Centre Tanga Salim Abdul Rahim Barahiyan kuwatukana maulamaa wakubwa wa Ah'li Sunna kwa kuwabandika tuhuma na kuwazulia mambo mengi ya uongo ambayo hawanayo na bila shaka hujuma hizo anazozifanya Salim dhidi ya maulamaa hao hazina budi kupigwa vita kwa hoja na dalili ili kuvikomesha vitendo hivyo viovu vinavyofanywa na mtajwa huyo na washirika wake.

Kama utakuwa ndugu msomaji umezifuatilia kwa kina makala zetu namba 13 na 14 na ukafanya uwiano baina ya makala hizo na ile mihadhara ya kash'fa iliyotolewa na Salim Barahiyan utayagundua malengo maovu ya mtu huyu dhidi ya maulamaa hawa,na pia utagundua kwamba ni mtu aliyefilisika kihoja.

Katika makala hizo mbili 13 na 14 tumetaja kauli za baadhi ya maulamaa wakubwa wa Ahli Sunna katika zama hizi kama vile;

1-Sheikh Muhammad Nasiru din al Albany mwanawachuoni mkubwa wa hadithi katika zama hizi bila ya mpinzani.

2-Sheikh Abdul Aziz Ibn Baaz aliyekuwa Mufti wa Saudi Arabia.

3-Sheikh Muhammad Swaleh Ibn Uthaimin ambaye ni mmoja katika jopo la maulamaa wakubwa wa Saudi Arabia.

4-Sheikh Ubaidillahi al Mubaarakfury katika maulamaa wa kisalafi bara Hindi.

5-Sheikh Muhammad Abdul Wahab al Banna miongoni mwa maulamaa wakubwa wa Makka.

6-Sheikh Swaleh Ibn Fawzan al Fawzan ni mmoja katika jopo la maulamaa wakubwa wa Saudi Arabia.

7-Sheikh Muhammad Ibn Abdillahi al Subail Imamu wa msikiti mtukufu wa Makka.

8-Sheikh Abdul Muhsin al Abbaad ambaye ni miongoni mwa maulamaa wakubwa wa Madina na ni mwalimu katika msikiti wa Mtume s.a.w.

Na wengineo katika maulamaa wakubwa wa Ah'li Sunna katika zama hizi.
Lengo letu katika kuzitaja kauli hizo za maulamaa hao wakubwa ni kuwataka watu wapime wenyewe baina ya matusi ya Salim Barahiyan dhidi ya Sheikh Rabii al Mad'khaly, Muq'bil Ibn Haadi Waadi'I na Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy,wayapime matusi hayo ya Salim Barahiyan na kauli za maulamaa hao wakubwa ambazo zinawasifu kwa sifa kemkem sifa ambazo zinathibitisha kwamba wao ni watu wenye elimu fadhla na msimamo mzuri na itikadi sahihi.

Ama makala hii namba 15 itamzungumzia aliyekuwa mwanachuoni mkubwa wa Sunna katika nchi ya Yemen MUQ'BIL IBN HAADI IBN MUQ'BIL AL WAADI'I ambaye pia hakupona na ufedhuli wa Salim Barahiyan.
Na bila shaka kusimama kulikemea jambo hili na kuwatia adabu wenye tabia hizo ni wajibu.

Na kabla sijaanza kumuelezea ninani MUQ'BIL ninamkumbusha Salim Barahiyan na wale wote wenye tabia kama yake kauli hii ya Allah s.w.t. pale aliposema;

وَلاَ تَحْسَبَنَّ اللّهَ غَافِلاً عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ.. ُ}

"Wala msidhani kwamba Allah ni mwenye kughafilika kwa yale wanayoyafanya madhalimu…." Surat Ibrahim 42.

Na pia ninamkumbusha kauli ya al Imamu Ibn Asaakir pale aliposema;

**"..أن لحوم العلماء رحمة الله عليهم مسمومة وعادة الله في هتك أستار منتقصيهم معلومة لأن الوقيعة فيهم بما هم منه براء أمره عظيم...."**

"..{Fahamu) kwamba nyama za maulamaa –Allah awarehemu-ni zenye sumu na kawaida ya mwenyezi mungu katika kuvunja sitira za wenye kuwatukana ni jambo lenye kujulikana na kuwatuhumu kwa yale ambayo wako mbali nayo jambo lake ni kubwa mno..".
tabyiinul kadhibil muftari 1/29.

Na sababu ambazo zimenipelekea kumzungumzia Sheikh Muq'bil al Waadi'i ni sababu zilezile tulizo zitaja katika makala namba 13 kuhusu Sheikh Rabii,nao ni upotoshaji wa haki dhidi ya Sheikh huyu uliofanywa na Mudir wa Ansaar Muslim Youth Centre Tanga Salim Barahiyan katika muhadhara wake aliokuwa akizungumzia kuhusa Salafiyya Jadidah!
Pale alipodai kwamba kuna kundi potofu linaloitwa Salafiyya Jadida kundi ambalo limeanzishwa na masheikh hawa;

1-Rabii al Mad khaly
2-MUQ'BIL IBN HAADI AL WAADI'I.
3-Yahya Ibn Ally al Hajuury mwanafunzi wa Sheikh Muqbil.

## NI NANI SHEIKH MUQ'BIL ?

Hii ifuatayo ni historia fupi ya Sheikh Muq'bil Ibn Haadi

### 1-Jina lake;
Muq'bil Ibn Haadi Ibn Muq'bil Ibn Qaa'idah al Hamdaani al Waadi'i.

### 2-Mahali alipozaliwa;
Sheikh Muq'bil amezaliwa katika kijiji cha Dammaaj katika mji wa Sa'adah kaskazini mwa nchi ya Yemen.

### 3-Masheikh wake waliomsomesha;

Hawa wafuatao ni baadhi ya masheikh waliomsomesha Sheikh Muq'bil;

1-Sheikh Abul Hussein Majdu din al Muayyid katika mji wa Najran kusini mwa Saudi Arabia.
2-Sheikh Muhammmad Ibn Sinaan al Hadday.

3-Sheikh Yah'ya Ibn Uthman al Baakistany katika msikiti mtukufu wa Makka amemsomesha Tafsir ya Ibn Kathir na Sahihi Bukhari na Muslim na Sheikh huyu bado yuko hai na anaendelea na darasa zake ndani ya msikiti mtukufu wa Makka.
4-Sheikh Abdul Aziz al Subayil Imamu wa msikiti mtukufu wa Makka.
5-Sheikh Abdallah Ibn Muhammad Ibn Humaid Imamu wa msikiti wa Makka,amesoma kwake elimu ya mirathi.
6-Sheikh Sayyid Muhammad Muhammad al Hakim al Masri.
7-Sheikh Mahmoud Abdul Wahab Faid al Masri.
8-Muhammad al Amin al Masri.
9-Sheikh Hamad al Ansaary al Khaz'rajy mwanawachuoni wa Hadithi katika mji wa Madina katika wakati wake.
10-Sheikh Abdul Aziz Ibn Baaz amesoma kwake Sahihi Muslim katika msikiti wa Mtume s.a.w.
11-Mwanawachuoni mkubwa wa Hadithi katika zama hizi Sheikh Muhammad Nasirud din al Albany.
Tazama kitabu chake Sheikh Muq'bil kiitwacho Tarjamatu Abi Abdil Rahman uk 21-25.

## 4-Wanafunzi wake;

Hawa wafuatao ni baadhi ya wanafunzi wake wakubwa na mashuhuri katika ulimwengu wa kiislamu;

1-Sheikh Yah'ya Ibn Ally al Hajuury Abu Abdil Rah'man,na yeye kwasasa ndiye aliyeshika mar'kaz ya Sheikh baada ya kufariki Sheikh.
2-SheikhUsaamah Ibn Abdil Latif al Quuswi Abu Hatim al Masri,yeye ana Markaz ya kisalafi mjini Cairo-Misri.
3-Sheikh Abdul Rahman Ibn Umar al Hadhramy ana markaz ya kisalafi katika mji wa Aden.
4-Sheikh Muhammad Ibn Swaleh al Swaumaly Imam wa Jaamil khair Sana'a.
5-Sheikh Abu Abdillah Mustafa al Adawy al Masri muandishi mashuhuri wa vitabu.
6-Sheikh Abu Nasri Muhammad al Imam Ibn Adillah al Raimy mwenye kitabu Tan'wirul dhulumaat kinacho zungumzia mas'ala ya ubatili wa Demokrasi na uchaguzi ana markazi kubwa ya kisalfi kule sehemu za Ma'abar-Yemen.
7-Sheikh Muhammad Abdul wahab al Abdaly al Wusabi Abu Ibrahim ana markaz ya kisalafi katika mji wa Hudaydah na ni muandishi mashuhuri wa vitabu.
Na wengineo wengi waliojaa katika kila kona ya dunia.

## 5-Vitabu alivyoandika;

Sheikh-Allah amrehemu- ameandika vitabu vingi mno katika fani tofauti na hivi vifuatavyo ni baadhi ya vitabu vyake;

1-al Sahihul Musnad min as'baabin nuzuul.
2-Uhakiki wa kitabu cha Imamu al Daaraqut'niy kiitwacho "al il'zaamaatu wat tatabu'u".ni kitabu chake alichopatia shahada ya pili.katika kitivo cha Hadithi chuo kikuu cha kiislamu cha Madinah.
3-al Sahihul Musanad mimmaa laisa fi Sahiihain.
4-al Makh'raju minal Fit'nah.
5-al Sahihul Musnadu min Dalaailin Nubuwah.
6-al Jaamius Sahihu fil Qadar.
7-I'laanun nakiir a'laa as'haabi I'dil Ghadir.
Na vinginevyo ambavyo vimejaa katika maktaba za kiislamu.

## 6-Kauli za maulamaa wa Sunna kuhusu Sheikh Muq'bil;

Kwahakika ni kwamba maulamaa wengi wa Ah'li Sunnat wal Jamaa wamemsifia sana Sheikh Muq'bil juu ya msimamo wa wake wa haki aliokuwa nao na juhudi kubwa aliyoifanya -baada ya tawfiq ya Allah- katika kueneza Sunna za Bwana Mtume s.a.w. hasa katika nchi ya Yemen,nchi ambayo ilikuwa imefunikwa na bid'a za kila sampuli.

Lakini hapa tutawataja maulamaa wachache tu waliomsifia mwanawachuoni huyu pamoja na kutaja baadhi ya kauli zao;

### 1-Sheikh Muhammad Swaleh Ibn Uthaimin Allah amrehemu,

Amesema Sheikh huyu;

"قولوا له أنا أعتبره مجدِّداً".

"Mwambieni (Sheikh Muq'bil)mimi ninamzingatia yeye kwamba ni Mujaddidi (amehuisha dini katika nchi ya Yemen).
Tazama kitabu nub'dhatun mukh'tasara cha Ummu Abdillahi Binti wa Sheikh Muq'bil uk 46.

### 2-Sheikh Rabii Ibn Haadi Ibn Umair al Mad'khaly,

Naye pia amesema kama alivyosema Sheikh Ibn Uthaimin,amesema;

"هو المجدد فى بلاد اليمن وأنه لا يوجد منذ زمن عبد الرزاق الصنعاني  إلى يومنا هذا من قام بالدعوة وجددها كالوادعي ".

"Yeye ni mujaddidi (amehuisha dini) katika nchi ya Yemen na hakupatikana tangu zama za Abdul Razaq al San'aany mpaka leo hii mtu aliyesimamisha da'awa na kuihuisha kama (Muq'bil) al Waadi'i".

3-Sheikh Ubeid Ibn Abdillahi al Jaabiry miongoni mwa maulamaa wa wakubwa wa Madina,na aliwahi kuwa mwalimu katika chuo kikuu cha Madina.
Nilipomuuliza sheikh huyu kuhusu masheikh hawa;
Muhammad Amaan al Jaamy,Sheikh Rabii,Sheikh Mq'bil,na Sheikh Muhammad Haadi,akasema Sheikh Ubeid;

".. ومنهج هؤلاء المشايخ - ولله الحمد- طيب الشيخ ربيع والشيخ محمد بن هادي والشيخ مقبل رحمه الله منهجهم ولله الحمد سليم.
لكن جرت عادة الإخوان المسلمين ومن تفرّع عنهم أنهم كل من يخالفونه يلقبونه بأبشع الألقاب ويصفونه بأبشع الأوصاف..".

"Muelekeo wa masheikh hawa ni mzuri,sheikh Rabii,sheikh Muhammad Haadi,na sheikh MUQ'BIL –Allah amrehemu- muelekeo wao umesalimika.
Lakini Ikh'wanul muslimina(Muslim Brotherhood) na wale waliozalikana nao ni kwamba wao kila wanaye tofautiana naye wanambandika jina baya,na kumpa sifa mbaya..".
Maneno haya yamo katika kanda ya maswali ya vijana wa kisalafi kutoka Tanzania kwenda kwa Sheikh Ubeid al Jaabiry.

4-Sheikh Muhammad Nasirud Din al Albany,

Sheikh Muhammad Naasirud Din al Albany r.a.yeye amesema baada ya kuulizwa swali;

((على الرغم من موقف فضيلة الشيخين ربيع بن هادي المدخلي ومقبل بن هادي الوادعي فى مجاهدة البدع والأقوال المنحرفة يشكك بعض الشباب فى الشيخين أنهما على الخط السلفي؟
فأجاب –رحمه الله -:
((نحن بلا شك نحمد الله –عز وجل – أن سخر لهذه الدعوة الصالحة القائمة على الكتاب والسنة على منهج السلف الصالح دعاة عديدين فى مختلف البلاد الإسلامية يقومون بالفرض الكفائي الذي قل من يقوم به فى العالم الإسلامي اليوم،
فالحط على هذين الشيخين الشيخ ربيع والشيخ مقبل الداعيين إلى الكتاب والسنة،وما كان عليه السلف الصالح ومحاربة الذين يخالفون هذا المنهج الصحيح هو كما لا يخفىعلى الجميع إنما يصدر من أحد رجلين:
إما جاهل،أو صاحب هوى.
الجاهل يمكن هدايته.....
أما صاحب الهوى فليس لنا إليه سبيل،إلا أن يهديه الله –تبارك وتعالى- فهؤلاء الذين ينتقدون الشيخين-كما ذكرنا
إما جاهل فيعلَّم،
وإما صاحب هوى فيستعاذ بالله من شره ،
ونطلب من الله –عز وجل – إما أن يهديه وإما أن يقصم ظهره)).
Aliulizwa Sheikh Al Bany swali lifuatalo;

"Sheikh  pamoja na msimamo waliokuwa nao masheikh hawa wawili Rabii Ibn Haady al Mad khaly,na Muq'bil Ibn Haady al Waadi'i katika kupambana na Uzushi na kauli zilizopotoka,baadhi ya vijana bado wanatia shaka kwamba masheikh hawa wako katika mstari wa Salafi?

Akajibu Sheik Al Bany kwa kusema;

"Sisi bila shaka yoyote tunamshukuru Allah s.w.t. kwa kuiwekea da'awa hii njema iliyosimama katika kitabu na Sunna juu ya ufahamu wa wema waliotangulia walinganizi wengi katika miji mbalimbali ya kiislam ambao husimama kutekeleza faradhi kifaya jambo ambalo ni wachache wenye kulifanya katika ulimwengu wa kiislamu hii leo.

Kuwatukana masheikh hawa wawili sheikh Rabii,na Sheikh Muqbil ambao wanalingania kwenye kitabu na Sunna kwa ufahamu wa wema walio tangulia,na kupambana na wale ambao wanaihalifu hii manhaji sahihi kama ambavyo haijifichi kwa wote kwamba jambo hili (la kuwatukana) halitoki ila kwa mmoja kati ya watu wa sampuli mbili;

IMA MJINGA!!!

AU MTU WA KUFUATA MATAMANIO!!!!

Jahili kuna uwezekano wa kumuongoza.
Ama mwenye kufuata matamanio yake hatuna njia ya kumfanya ila kumuomba Allah amuongoze.
Kwahiyo hawa ambao wanawatukana hawa masheikh wawili-kama tulivyotangulia kutaja-
mjinga ataelimishwa.
na mwenye matamanio ya nafsi tunamuomba Allah atulinde na shari yake,
ima amuongoze AU AUVUNJE MGONGO WAKE". Mwisho wa kunukulu.
Silsilatul hudaa wan nour cassette namba851/1 swali liliulizwa tarehe 9/7/1416h,na Abul Hassan al Ma'ariby.na kitabu athanaul badi'u uk17-18.

Hebu ndugu msomaji tuyatafakari maneno ya mwanawachuoni huyu kwa kina juu ya Sheikh Muq'bil kisha tuyalinganishe na matusi ya Salim Barahiyan dhidi ya Sheikh Muq'bil.

Kwa muh'tasari ni kwamba;

Sheikh Albany anamzingatia Sheikh Muq'bil ni katika maulamaa wa Ah'li Sunna mwenye kulingania katika man'haji ya Salafi.

Salim Barahiyan anasema kwamba Sheikh Muq'bil analingania kwenye Salafiya Jadida-kama anavyodai- bali ni katika waanzilishi wa kundi hilo potevu!!!

Sheikh Albany anasema kwamba haifai kuwatukana masheikh hawa (Rabii na Muq'bil) na mwenye kuwatukana ima atakuwa ni mtu mjinga anatakikana aelimishwe au mtu anaye fuata matamanio yake.

Salim Barahiyan anawatukana masheikh hawa wawili hadharani na kuwatuhumu eti wamekuja na fikra mpya na kundi jipya la Salafiya Jadida?!!

Sheikh Albany –Allah amrehemu- anaomba dua kwamba hawa wanao watukana masheikh hawa (Rabii na Muq'bil) kama huyo anayefanya hivyo ni mjinga basi Allah amuongoze.
Na kama ni mtu wa anayejua lakini anafuata matamanio yake basi Allah atulinde na shari zake ima Allah amuongoze au AUVUNJE MGONGO WAKE!!!
ALLAHUMMMA AAMIIN !!!

Na bila shaka dua hii ya mwanachuoni huyu haitamkosa Salim Barahiyan kwa ujeuri,ufedhuli na kiburi anachokifanya dhidi ya masheikh hawa wa Sunna.

Sasa huo ndio msimamo na mtazamo wa Muhaddith wa zama hizi Sheikh al Allaamah Albany Allah amrehemu juu ya maulamaa hawa je wewe Salim Abdul Rahim na huyo kijana aliyekuwa muajiriwa mwenzako Abu Hamza kutoka Chundwa mnasemaje?

Si ndiyo tukasema kwamba Albaany kwako wewe Salim Barahiyan na wafuasi (wanachama) wako ni Sheikh wa kutegemewa katika Swala na Swaumu ya Jumamosi na kuweka au kutokuweka ubao kaburini?
Na mkataka kufanya mijadala na watu juu ya mas'ala haya! Hivi sasa ndiyo mnajidai oh' Salaf walitofautiana lakini hawakufarikiana?!!

Na maneno haya anayakariri sana kijana mmoja mashuhuri kule Arusha kwa kazi ya uganga wa kutoa majini kwa jina anaitwa Sudi,mimi nasaha

zangu kwake atafute mahali akasome dini,hata kama ana shahada ya kutoa majini bado analazimika kusoma.
Kwani naye pia ukimsikiliza pale anapozitoa aya za Qur'an anazitwanga –Laa hawla illaa billaah-hata sijui hilo zinguo analisoma vipi!!!?

Kwa ufupi wa maneno ya Sheikh Albany ni kwamba mtu kama Salim Barahiyan na wenzake wanaowatuhumu maulamaa hawa;

Ima ni majahili(wajinga) basi waelimishwe na hii ndiyo kazi tunayoifanya sisi katika makala hizi.

Au ni watu wenye kufuata matamanio ya nafsi zao kwa kutaka ukubwa wa dunia Allah atukinge na shari zao na awavunjilie mbali,na bila shaka Salafi yoyote ataitikia Aamiin.

Ndugu msomaji huyo ndiye Sheikh Muq'bil kwa mtazamo wa Sheikh Albany na kwa mtazamo wa maulamaa wa Sunna walio juu man'haji ya Salaf.

7-Mauti yake;

Sheikh Muq'bil Allah amrehemu amefariki usiku wa Jumapili 2/Jumaadal Uulaa/1422H sawa na 21/7/2001 M,katika mji wa Jeddah-Saudi Arabia akiwa na umri takriban miaka Sabini.

Na aliswaliwa katika msikiti wa Makkah baada ya swala ya al faj'ri na kuzikwa katika makaburi ya Al Ad'li jirani na kaburi la Sheikh Abdul Aziz Ibn Baaz na Sheikh Muhammad Ibn Swaleh Ibn Uthaimin- Allah awarehemu maulamaa wetu na atukutanishe nao katika Firdawsil a'alaa-Aamiin.

## Msimamo wa Sheikh Muq'bil dhidi ya serikali ya Saudi Arabia

Sheikh Muq'bil -Allah amrehemu- alikuwa ni miongoni mwa maulamaa wa Ah'li Sunna katika zama hizi waliosimama katika njia sahihi ya Salaf, Lakini yeye ni mwanaadamu hupatia na hukosea kama ilivyo kawaida kwa wanaadamu wote.

Lakini pamoja na kukosea kwake huko hakuna hata mwanachuoni mmoja wa Ah'li Sunna aliyemtoa katika njia sahihi ya Salaf,bali alinasihiwa na hatimae kurudi katika njia ya sawa ya Salaf kama ilivyo mashuhuri kwa maulamaa wa kisalaf wanapoteleza ni wepesi kurudi katika haki.

Sheikh alikuwa mkali mno dhidi ya watawala hasa wa nchi za kiislamu kama vile Saudi Arabia na aliwahi kuandika vitabu na kutoa mihadhara mikali dhidi ya serikali ya Saudi Arabia na mfalme wa nchi hiyo kwa wakati huo ambaye ni Mfalme Fah'd Ibn Adul Aziz -Allah amrehemu- hasa pale lilipotokea tukio la mfalme huyo kuvishwa msalaba kwa hadaa kule nchini Uingereza!

Lakini Sheikh Muq'bil aliponasihiwa kuhusu kadhia hii kwamba si katika utaratibu sahihi wa Salaf kuwatukana na kuwanasihi watawala hadharani bali hiyo ni sera ya makhawariji watu wa fujo kwa muda mrefu Sheikh hakukinaishwa na nasaha hizo.

Lakini mwisho wa umri wake kabla ya kufa kwake Sheikh alitoa kauli ya wazi na kutangaza toba hadharani na kuubatilisha msimamo aliokuwa nao,na maneno haya yamerekodiwa katika kanda iitwayo kwa jina la Mushahadaatii fil Mamlakatil Arabiyyati Suudiyyah (niliyo yashuhudia katika nchi ya Saudia) na pia kwenye kitabu chenye jina hilo vilevile kwenye Cd na kutafsiriwa kwa lugha tofauti ikiwemo lugha ya kizungu.

Ama kitendo kiovu kilichofanywa na Salim Barahiyan cha kumtukana Sheikh huyu na kumtuhumu kwa tuhuma tele na kuufananisha msimamo wa Sheikh huyu na Boss wake Muhammad Surur anayeshi Uingereza hadi sasa -na huwenda akawa anatumiwa na makafiri ili kuwapotosha watu- ni kitendo ambacho kinadhihirisha wazi ujahili wake au kufuata kwake matamanio ya nafsi yake.

Vipi utamfananisha mtu ambaye maulamaa wa Sunna wanakiri kuwa ni mwanawachuoni aliyesimama katika haki na kuipigania Sunna juu ya njia sahihi ya wema waliotangulia bali wengine wamemzingatia kuwa ni mujaddid ? hebu soma kwa makini maneno ya Sheikh Albany na Ibn Uthaimin hapo nyuma utaligundua hilo.

Vipi utamfananisha mwanachuoni huyo na Boss wako ambaye maulamaa wamemuita kwamba ni katika walinganizi wa batili?
Soma maneno ya Sheikh al Fawzan katika kitabu cha fatawa zake al aj'wibatul mufidah uk 80-90.
Sikiliza kanda ya muhadhara wa Sheikh Ibn Baaz iitwayo Aafaatul lisaan(maafa ya ulimi).

Vipi wewe Salim Barahiyan utamlinganisha mwanawachuoni wa Sunna aliyemaliza umri wake katika kuhuisha na kuwaelimisha watu itikadi sahihi ya Ahli Sunna na ikatangaa elimu hiyo kwa fadhla za Allah katika

kila kona ya dunia! Hebu soma maneno ya Sheikh Ibn Uthaimin na Sheikh Rabii hapo nyuma utaling'amua hilo.

Vipi wewe Salim Barahiyan utamfananisha Sheikh huyu na mtu ambaye anaishi katika kasri huko nchini Uingereza chini ya kivuli cha makafiri hatujui malengo yake nini! Yeye kazi yake ni kuvikashifu vitabu vya Tawheed na kuwatukana maulamaa wa Ah'li Sunna kupitia Gazeti lake aliloliita Gazeti la Sunna ambalo sheikh Albany na Sheikh Muq'bil wanaliita Gazeti la Bid'a!!!

Fuatilia marejeo tuliyoyataja hapo juu na kwa ziada soma kitabu al Qutbiyya cha al Ad'nany kuyathibitisha haya ninayo yasema.

## Kuufichua uongo wa Salim Barahiyan

Kutokana na ubabaishaji na uongo mwingi unaoenezwa na Salim Barahiyan pamoja wafuasi wake juu ya daawa ya Salaf Swalih tumeonelea katika makala hii tuweke ukurasa maalumu wa kufichua uongo huo kwa lengo la kuyaweka sawa baadhi ya mambo.

Kwahakika ni kwamba Salim Barahiyan amefilisika kwa hoja kama tulivyo tangulia kueleza huko nyuma,na hana jawabu za kielimu za kuvunja hoja yoyote miongoni mwa zile tulizozitoa ili kuupa ukweli uchukue nafasi yake,kwahiyo silaha kubwa anayoitumia hivi sasa ni ubabaishaji na uongo.

Na hii hapa ni mifano michache ya uongo wake kati ya mingi;

**Uongo wake wa kwanza;**

1-Ni pale anapomtuhumu Sheikh Rabii kwamba anamzulia Sayyid Qut'bi juu ya itikadi ya wihdatul wujud (kila kitu ni mungu na mungu ni kila kitu).

Jawabu yetu;
Sisi katika makala namba 13 tukamuelimisha kwamba Sheikh Rabii hakumzulia Sayyid Qut'bi ukweli kwamba maneno yake Sayyid Qutbi katika tafsiri yake iitwayo "fi dhilalil Qur'an" yanaishiria hivyo kama ilivyo katika tafsiri ya surat al Hadid na surat al Ikh'laas.

Pia si Sheikh Rabii peke yake aliyeyasema hayo juu ya Sayyid Qut'bi,bali hiyo ndiyo kauli ya AlBany,Ibn Uthaimin,Abdallah Duweish na wengineo katika maulamaa wa kisalafi,amesema Sheikh AlBany;

**"نقل سيد قطب كلام الصوفية ولايمكن أن يفهم منه إلا أنه يقول بوحدة الوجود".**

**انظر: برآءة علماء الأمة ص 42.**

"Ameyanukulu Sayyid Qut bi maneno ya masufi.na haiwezikani kufahamika maneno hayo ila kuwa Sayyid anasema wih'datul wujuud".

Tazama kitabu baraatu ulaamail umma uk 42.

Na amesema sheikh Ibn Uthaimin;

**"قرأت تفسيره – يعني فى ظلال القرآن لسيد قطب- لسورة الإخلاص،وقد قال قولا عظيماً فيها،مخالفاً لما عليه أهل السنة والجماعة، حيث إن تفسيره لها يدل أنه يقول بوحدة الوجود".**

"Nimeisoma tafsiri yake-Fi dhilalil Qur'an ya Sayyid Qut bi- katika suratil Ikhlas,kwahakika amesema maneno makubwa yenye kuhalifiana na yale waliyo nayo Ahli Sunna wal Jamaa!!.

Kwahakika katika tafsiri yake ya sura hiyo anasema kauli ya wihdatul wujuud".

Tazama kitabu baraatu ulamail umma uk 42.

Kwahiyo tunamnasihi tuhuma zake hizo pia azielekeze kwa masheikh hawa na aseme kwamba hawa pia ni Salafiya Jadidah!

Mbona lawama zinaelekezwa kwa Sheikh Rabii pekeyake? Je hiyo ndiyo insafu au kuna agenda ya siri dhidi ya Sheikh huyu? Bila shaka uongo wake huu umebainika.

**Uongo wake wa pili;**

Salim Barahiyan katika kudhihirisha chuki zake dhidi ya Sheikh huyu na akataka kuzipandikiza chuki hizo kwa wafuasi wake ambao wengi wao hawana taaluma yoyote ya dini alizua uongo ufuatao;

Anadai kwamba Sheikh Rabii amefukuzwa Madina eti kwasababu amemtukana/amemkandia Sheikh mmoja wa kabila la ki Shinqitwy!!

na anadai kwamba ameambiwa na mwalimu (Mudir) wa chuo cha Imam Shaafy Sahare Tanga ambaye ni muajiriwa wake Ustadh Ally Nassor-akamtaja wazi mwalimu huyo-.

Jawabu yetu;

Huu ni uongo ambao Salim Barahiyan na mahiz'bi wenzake wanauendeleza dhidi ya maulamaa wa kisalaf,na kwahakika hawatofaulu.

Na hapa tunaufichua uongo huo kwa kuhoji kama ifuatavyo;

1-Vitabu vya Sheikh Rabii ni maarufu na tuko navyo,kanda na cd zake zimejaa tele maneno yake katika web site ya http//sahab talk.net na nyinginezo kwa kiarabu na kizungu yamejaa tele,basi tutajiwe ni kauli gani hiyo aliyoitoa Sheikh Rabii juu ya huyo Sheikh wa kishin'qitwi iliyompelekea kufukuzwa Madina? tena tutajiwe maneno hayo yako mahali gani?

Maana mimi ninaifahamu kauli ya Sheikh Rabii juu ya Sheikh huyo na niko nayo kwa sauti yake hasa na si kauli ya kumfanya mtu mfano wa huyo mudir wa chuo cha Imam Shaafy kufukuzwa Madina seuze Sheikh Rabii!

2-Sheikh Rabii ana ratiba ya mihadhara katika mji wa Madina kila mara na mimi kipindi niko Madina nimeshawahi kuhudhuria mihadhara yake katika Masjidi Qubaa zaidi ya mara moja,muhadhara wa mwisho kuhudhuria mimi ni pale ilipotokea fit'na ya Abul Hassan al Ma'aribi mwaka 2002 2003 maulamaa wa Madina walikaa akiwemo Sheikh Rabii kuijadili kadhia hiyo kisha Sheikh Rabii akafanya muhadhara kuhusu kadhia hiyo masjid Qubaa na mimi nilihudhuria muhadhara huo.

Swali kama amefukuzwa Madina kwasababu ya kumsema Sheikh fulani wa Madina –jambo ambalo ni uongo- mbona bado anaendelea kutoa mihadhara yake ndani ya mji mtukufu wa Madina na kutangazwa rasmi kiserikali tena katika misikiti iliyo chini ya mamlaka ya serikali kama vile masjid Qubaa?

3-Bali Sheikh Rabii amewarudi masheikh wakubwa zaidi ya Sheikh huyo kielimu na umri -kama ilivyo katika misingi ya Ah'li Sunna kumrudi kila anayekwenda kinyume- amewarudi baadhi ya masheikh walioko Makka,Madina,Riyadh,ndani ya Saudia na nje ya Saudia mbona hatujasikia kwamba Sheikh Rabii au mwingineo amefukuzwa kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine?

Lakini yote haya yanatubainishia msimamo potofu aliokuwa nao Salim Barahiyan na washirika wake na utovu wa adabu waliokuwa nao dhidi ya maulamaa wa Sunna.

**Uongo wake wa tatu;**

Pia alimtuhumu Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy kwamba alisema maneno ya kujipendekeza kwa selikali ya Saudia ili apate uraia wa nchi hiyo!!
Jawabu yetu;
Na huu pia ni uongo mkubwa tena uliojaa ukosefu wa adabu dhidi ya mwanawachuoni huyu mkubwa aliyekuwa mwalimu katika msikiti wa Mtume s.a.w. huko Madina.

Bali ukweli ni kwamba Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy kauli aliyoitoa ndiyo ileile iliyotolewa na jopo la mulamaa wakubwa wa Saudi Arabia k.v.Ibn Baaz,Ibn Uthaimin,al Fawzan,al Ghudayyaan,al Luhaidaan na wengineo miongoni mwa maulamaa hao wakubwa,sasa na wao walikuwa wakijipendekeza ili wapewe nini?

Lakini kitendo hiki cha kuwatukana maulamaa hawa kwamba ni maulamaa wanaotumikia mas'lahi ya serikali(vibaraka) ni kitendo kinachoenezwa na wazushi akiwemo Muhammad Surur Boss wake Salim Barahiyan anayeishi Uingereza!

Hebu yazingatie haya maneno ya Boss wa Salim kuhusu maulamaa wa Saudi Arabia halafu uyalinganishe na maneno yake juu ya Sheikh Muhammad al Jaamy,amesema Boss wake huyo;

"Kuna kundi jingine ambalo linachukua misaada rasmi (ya serikali) na wanaifungamanisha misimamo yao na misimamo ya mabwana zao…

Mabwana wakitaka msaada kutoka Marekani watumwa wanasimama kuzikusanya dalili ambazo zinahalalisha jambo hili…tofauti zikiisha watumwa nao wananyamaza…kundi hili linasema uongo…linafanya ujasusi …hata kama **watarefusha ndevu zao na kupunguza nguo zao** na wakadai kwamba wao ni watetezi wa Sunna lakini daawa ya kiislamu haidhuriki kwa kupatikana kundi hili la watu kwasababu **UNAFIKI NI WA KALE**…".

Tazama Gazeti lake analoliita "Sunnah" -Sheikh Muq'bil anasema Gazeti hili linastahiki kuitwa Gazeti la bid'a-! Gazeti hilo namba 23 la mfunguo tatu(Dhul Hijjah) mwaka 1412 uk 29-30.

Bila shaka Salim naye anaendeleza fikra za Boss wake!!!!

Ama kuhusu suala la uraia wa Sheikh Muhammad al Jaamy ukweli ni kwamba Sheikh alikuwa ni raia wa Saudi Arabia kabla ya tukio hilo kwa miaka arobaini na hiyo ndiyo kauli iliyo na nguvu (kabla hata Salim

Abdul Rahim hajazaliwa)!!! miaka 40 kabla ya mwaka 1991 mpaka leo ni miaka mingapi? Je yeye Salim Barahiyan ana miaka mingapi? Sasa kwanini afanye utovu wa adabu?

Napia tumuulize Salim Barahiyan anakusudia nini juu ya uongo wake huu? Na je anataka kuifahamisha nini jamii ya kiislamu na wasio kuwa waislamu kuhusu Sheikh huyu?

Je hiyo si dalili ya kupinda kwake? Je hayuko katika kutumikia malengo ya Boss wake aliyeko Uingereza? Na je huo si utovu wa adabu?
Na bila shaka mpaka hapa ndugu msomaji utakuwa umeubaini uongo wa Salim Barahiyan na ubabaishaji wake.

Lakini jambo kubwa ambalo linawashangaza wengi walio katika msimamo sahihi na wa haki wa Salaf Swalih (msimamo wa wema walio tangulia) ni kitendo cha Salim Barahiyan kuwatukana maulamaa wa Sunnah na kuwatetea kwa hoja nyonge watu wa bid'a kama Sayyid Qut'bi na wazandiki ambao maulamaa wamefikia kiwango cha kuwatoa katika uislamu kama Ibn Sina.

Pengine mtu mwenye ufahamu sahihi na insafu na kutaka kujua ukweli wa mambo ulivyo anaweza kujiuliza kila mara;

Kwanini Salim Abdul Rahim Barahiyan ameamua kuwakosea adabu maulamaa kama kina Muq'bil na kuwapa tuhuma kwamba ni watu wamekuja na fikra potofu na niwaanzilishi wa kundi potovu (Salafiya Jadida)?

Pia mtu anaweza kujiuliza swali hili;
Kama ni kweli kwamba maulamaa kama kina Muq'bil,Rabii na al Jaamy ni watu waliokuwa na itikadi potofu fikra potofu na ni waanzilishi wa kundi potofu inakuwaje kwa maulamaa kama AlBany Ibn Baaz,Ibn Uthaimin,al Fawzan,al Abbaad,al Subail na wengineo wawazingatie kwamba ni wenzao katika msimamo na hawafai kusemwa vibaya mpaka baadhi yao -k.v. Al Bany- kufikia kuwaombea dua mbaya wale wenye kuwataja kwa ubaya masheikh hawa ?!

Pia katika mambo muhimu ya kujiuliza ni haya;
Mbona Salim Barahiyan pale anapowatuhumu maulamaa hawa hataji hoja za kielimu zilizo wazi zinazowatoa maulamaa hawa katika mstari wa haki na kuwatia katika upotevu? Na badala yake anababaisha tu? Anataka kuufahamisha nini umma wa kiislamu juu ya maulamaa hawa?

Lakini pamoja na ufedhuli,kash'fa,uongo na uzushi unaofanywa na Salim Barahiyan bado kuna watu eti ambiwa hawafurahishwi na sisi kumkemea Salim Barahiyan kwa madai ya kwamba tuna sababisha farka,watu wameshaanza kuwa kitu kimoja! jamani mwatupeleka wapi? Sisi sote ni watu wa sunna mbona hivi ?!!!

Maswali yetu kwa hawa walio na vilio hivi vya uongo ni haya yafuatayo;

1-Je kwenu nyinyi ni fahari kubwa sana Salim Barahiyan kuwatukana maulamaa wa Sunna kama Muq'bil,Rabii,al Jaamy? Je ni umoja gani huo mnaoulinda mpaka muyafumbie macho matusi haya kwa maulamaa?au maulamaa kwenu nyinyi si chochote?

2-Salim Barahiyan anasema katika kanda yake ya kikao na wafuasi wake wa jimbo la Mirerani mnamo tarehe 10/12/2006 na kanda hiyo mimi ninayo anasema kwamba watu wa Sunna hapa Tanzania tumefarikiana na sababu ya kufarikiana kwetu ni DUNIAA!!!
Swali;
Sasa ni umoja upi mnaoulilia nyinyi na hali dunia inashuhudia kwamba hamko pamoja?
Tena baya zaidi hata walimwengu wanashuhudia kwamba kilichowagawa ni dunia!!!

Kwani hamjui kwamba sisi waislamu tunaungana kwa ajili ya Allah na kufarikiana kwa ajili ya Allah tu?
Sasa ninani wa kulaumiwa baina ya waliofarikiana kwasababu zao za kidunia na wale waliofarikiana kwasababu ya kuisimamisha haki na kuwatetea maulamaa wa haki? Nielezeni kwa elimu mkiwa nyinyi ni wakweli!

Basi mjue kwamba siku zote watu ambao hufarikiana kwasababu ya mas'lahi yao binafsi hupatana vilevile kwa mas'alhi yao binafsi na hakuna dini hapo.

Na ama baadhi ya watu kudai kwamba sote ni wanasunna ya nini malumbano? Mimi ninawaomba warejee muhadhara wa Salim Barahiyan anaozungumzia salafiya jadidah watagundua kwamba sisi siyo kitu kimoja kwa mtazamo wa Barahiyan,maana hiyo salafiya jadidah ni kundi potovu!na nyiny hammo katika upotovu huo!
Kisha tunapo taka mjadala mwajidai sisi nikitu kimoja!! kwani na nyinyi pia salafiya jadidah? Acheni uongo na ujabani(uoga).

Na wengine wakakosa haya wakasema kwamba hawa wana ugomvi wao binafsi! Kipo wanachogombea wanagombea matajiri!!

Bila shaka wanao yasema haya wanahitajika kuleta ushahidi wa madai yao haya ya uongo na wasipofanya hivyo basi wajue kwamba kuna siku ya Qiyamah wataulizwa.

Na je katika makala zetu -zaidi ya kumkunja na kumvunja Salim Barahiyan kwa Aya na Hadithi na kauli za Maulamaa- wameshawahi kusikia kwamba tunataja kiwanja au gari,au shamba au mshahara???
Mcheni mola wenu na kuweni katika wakweli.

Na yeye mwenyewe (Salim Barahiyan) akawa anajihami kwa kusema;

Kijana huyu anataka kuiua Taasisi yetu,kwani kuna Taasisi ngapi hapa Tanzania mbona hatumsikii akizikandia?!

Ameapa kwamba ataisambaratisha ANSAAR MUSLIM YOUTH CENTRE akirudi kutoka masomoni!!!

Kijana ana hasadi kwasababu mimi ninakubalika na watu kama nini hapa Tanzania yeye hataki hilo!!!

Kwanza kabisa haya yote anayo yasema ni uongo mtupu,
Nataka ufahamu ndugu yangu kwamba kuna sababu nyingi zilizopelekea kumchapa Salim Barahiyan na Taasisi yake,na hapa nitazitaja sababu mbili tu;

1-Yeye na rafiki yake Abu Hamza ndiyo waliojifanya kimbelembele katika kuipiga vita Man'haji sahihi ya Salaf Swalih katika mihadhara yao ya wazi,na mmoja katika mihadhara hiyo ni ule uliofanyika pale Markaz kuu AMYC walipokuja Abu Hamza na Bahero kutoka Kenya wakielekea Lindi kwenye Kongamano la mwaka 2006.

2-Yeye ndiye anaye watukana maulamaa wa Salafi kama vile Sheikh Rabii,Muhammad Amaan al Jaamy na Muq'bil al Waadi'i.
Na kuwatetea mulhidina na mazandiki kama vile Ibn Sina na ndiye mwenye sera za bid'a katika taasisi yake sera za baia uanachama na nambari za uanachama mwanachama hai na maiti na ukimuhoji anatoa hoja kwamba wao ndiyo HIZ'BOLLAH na kutoa aya juu ya uongo wake huo.

Na kabla ya kufikia mwisho ya makala hii Salim Barahiyan baada ya kufilisika kwa hoja anaanza kukimbilia kutaja mambo binafsi,na kama kawaida yetu sisi tunasema hatuna nafasi ya kujibu tuhuma binafsi kwasababu waislamu hawatopata faida yoyote,na pia atakayeumbuka ni yeye Salim.
Kwamfano yeye anasema;
"wamekusanya vijana wadogo walio na umri wa kwenda shule lakini hawapelekwi shule na hili ni kosa la jinai..".

Tafsiri ya maneno yake haya ya fitina anaiambia serikali kwamba waje watushtaki na ikiwezekana madrasa yetu inayosomesha dini ifungwe kwa madai ya kwamba kuna watoto hawakupelekwa shule wanasomeshwa Qur'an tu na maneno ya mtume s.a.w.!!

Je waislamu mmemuelewa Salim Barahiyan? Bila shaka mmemuelewa siku nyingi,na je mmeielewa kazi yake?

Sasa hebu tusawazishe kidogo ili mpate kuubaini uovu wa mtu huyu;

1-Ni kweli Katika madrasa yetu watu wanasoma sana dini tu,na hatuna mchezo -walilllahil hamdu - Qur'an na Sunna na masomo mingineyo kama aqidah,na nahwu mustalahul hadithi tunayapa kipaumbele sana.

2-katika madrasa yetu wapo wanafunzi wanaosoma shule za sekondari msingi na wengi wao wanasoma shule ya al nour Pongwe pia tunao mpaka waalimu wanaosomesha shule wanaokuja kusoma na hakuna aliyemzuia mtu kusoma au kusomesha masomo ya dunia.

3-Sisi tuko tayari serekali na waislamu wafanye utafiti juu ya hilo lakini wakimaliza hapo tutawaelekeza chuo kimoja cha kuhifadhisha Qur'an kilichopo katika kanda ya kaskazini ambacho kiko chini ya usimamizi wa taasisi ya Salim Barahiyan ambacho kimekusanya watoto zaidi ya arobaini ambao wana umri wa kwenda shule lakini hawakupelekwa!
Swali je waislamu kufanya hivyo mnafurahi? kama si uhasidi ninini?
**Kama nyumba yako ni ya vioo usiwatupie watu mawe…!!!**

Sasa waislamu wanapata faida gani juu ya maneno yake haya ya kipuuzi? ndiyo maana sisi hatuko tayari kujibu tuhuma na maneno binafsi ambayo ndiyo wimbo wake katika mihadhara yake baada ya kufilisika kwa hoja.

Pia anadai kwamba tumewashawishi watu wawatoe watoto wao katika shule yake ya Avicenna (Ibn Sina) ili kuua juhudi za taasisi yake!

Sisi tunamwambia aache kusema uongo na kuropoka ovyo akitaka tumueleze sababu zilizo wafanya baadhi ya wazazi kuwatoa watoto wao sisi tutamueleza wazi kupitia makala tena kwa ushahidi,kwanini wazazi hao wawatoe watoto wao na bila shaka yeye na wafuasi wake hawataridhika na kutajiwa mambo hayo machafu na ya aibu yaliyotokea kwa watoto wa shule hiyo.

Lakini kwanini tufikie huko nasisi tumeamua kuwasitiri?basi muwe na adabu,mkisimama mseme maneno ya dini tena kwa hoja na si kuwapotezea waislamu muda wao kwa kuwapa maneno ya uongo ambayo lengo lake ni kuleta chuki na uadui.

## KHATIMA

Mwisho katika kuhitimisha makala hii baada ya kuiusia nafsi yangu kumcha Allah pia ninamuusia Salim Abdul Rahim Barahiyan na wafuasi wake na wasaidizi wake na wapambe wake wamuogope Allah na wajue kwamba nyama za maulamaa zina sumu kama anavyosema al Imamu Ibn Asaakir Allah amrehemu.

Pia ajuwe kwamba hawatukani maulamaa waliosimama katika msimamo wa haki isipokuwa mmoja kati ya hawa;
1-Mnafiki.
2-Fasiki (mtu muovu).
3-Au Hiz'biyun (Ima Ikh'wan au Qut'biyuun, Suruuriyun, n.k.).
Na mimi nina uhakika kwamba Salim Barahiyan hatoki nje ya watu watatu hawa.
Kama anavyosema Sheikh al Fawzani;

لا يقع على العلماء المستقيمين على الحق إلا أحد الثلاثة :
-إما منافق معلوم النفاق
-وإما فاسق يبغض العلماء لأنهم يمنعونه من الفسق .
-وإما حزبي ضال يبغض العلماء لأنهم لا يوافقونه على حزبيته وأفكاره المنحرفة

“Hawatukani maulamaa walio katika mstari wa sawasawa isipokuwa mmoja kati ya watu watatu;
-Ima atakua ni mnafiki anayejulikana kwa unafiki.
-Ima atakua ni mtu muovu anaye wachukia maulamaa kwasababu wanamkataza uovu wake.

-Ima atakua ni hiz’by (mtu wa vyama vya bid’a) aliyepotea anawachukia maulamaa kwasababu hawaafikiani naye katika bid’a yake na fikra zake zilizopinda”.
Tazama al aj’wibatul mufida uk 75.

Pamoja na kumtaarifu kwamba Inshaallah kila atakayesimama kumuunga mkono juu ya batili yake hii ya kuwatukana maulamaa hawa wa haki na kuipotosha Man'haji Sahihi katu hatutomuachia.

Sisi –INSHAALLAH-tutaitetea man'haji (njia) sahihi ya Salaf na maulamaa waliosimama juu ya man'haji hii kwa kiasi Allah alichotuwezesha katika elimu na mali,kwahiyo wafe wenye chuki na chuki zao na Allah yupamoja nasi.

Sisi katu hatuogopi lawama za wenye kulaumu wala uongo wa Salim Barahiyan na washirika wake waliomzunguka kwa ajili ya maslahi yao ya dunia!! akiwapa wanafurahi na akiwanyima wanaanza kumkimbia na kumtukana !!!
Bali sisi tutaangalia haki iko wapi tuifuate…

Kwa faida zaidi fuatilia mfululizo wa makala zetu hizi;
-Upambanuzi juu ya hukumu ya picha.
-Mtazamo wa Salaf juu ya Baia
**Mjue Imam wa Hadithi wa Yemen katika zama hizi Muq bil al Waady**
ndiyo hii iliyo mikononi mwako
Ni kina nani Salafiy Jadida?
Kuwaheshimu maulamaa majibu na maelezo.
(Makala maalumu kwa ajili ya naibu wake Salim Barahiyan)
Itikadi za Sayyid Qut'bi na Hassan al Banna kwa mtazamo wa sheria.
Ikh'wanul muslimina katika mizani ya Sunna.
Nb;
**ukiipata makala hii toa copy nyingine ili kueneza ujumbe,Allah atakupa ujira wa kutangaza kheri.**

**وبالله التوفيق**

**وصلى الله وسلم وبارك على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين**